

ੴ

Japuji Sahib

safari kuelekea kiroho
tafsiri ya kiswahili

orodha ya banis

| | |
|---|----|
| 1. Japuji Sahib----- | 1 |
| 2. maombi----- | 35 |
| 3. falsafa ya safari----- | 39 |
| 4. jukumu la wanawake----- | 41 |
| 5. umuhimu wa kilemba----- | 45 |
| 6. unyenyekevu ndio kiini kikuu katika safari yako--- | 47 |



We are distributing Free Gutkas, Divine message of the Guru globally in all the major languages, To Continue this Monumental task, please donate at <https://sggsonline.com/donation>

This Sewa has been done by Sewadars & SikhBookClub.

This text is only a translation and only gives the essence of the Guru's Divine word. For a more complete understanding, please read the Gurumukhi Sri Guru Granth Sahib Ji. If any errors are noticed, please notify us immediately via email at walnut@gmail.com.

Publisher: SikhBookClub.com

੧੯

Kuna Mungu mmoja wa milele kote duniani.

ਸਤਿਨਾਮੁ

Jina lake linaishi milele

ਕਰਤਾ ਪੁਰਖੁ

Mungu ni muumba wa vyote, na yuko kila mahali

ਨਿਰਭਉ

Mungu hamuogopi yeyote kwa kuwa hakuna mwenye nguvu kumshinda.

ਨਿਰਵੈਰੁ

Mungu hana ubaguzi

ਅਕਾਲ ਮੂਰਤਿ

Mungu yuko hai kila wakati, usiku na mchana.

ਅਜੂਨੀ

Mungu hawezi akafa wala kuzaliwa tena.

ਸੈਭੰ

Mungu hakuumbwa, na amejaa nuru.

ਗੁਰ ਪ੍ਰਸਾਦਿ ॥

Anaweza tu kutambulika kupitia kwa neema yake Guru.

॥ ਜਪੁ ॥

Imba na kutafari

ਆਦਿ ਸਚੁ ਜੁਗਾਦਿ ਸਚੁ ॥

Amekuwepo tangu mwanzoni mwa nyakati.

ਹੈ ਭੀ ਸਚੁ ਨਾਨਕ ਹੋਸੀ ਭੀ ਸਚੁ ॥੧॥

Mungu ni wa kweli leo, na atabakia kuwa wakweli katika siku za baadae.

ਸੋਚੈ ਸੋਚਿ ਨ ਹੋਵਈ ਜੇ ਸੋਚੀ ਲਖ ਵਾਰ ॥

Kutakasa maeneo ya hija haifakii usafi wa akili, hata kama itafanywa mara zaidi ya milioni moja.

ਚੁਪੈ ਚੁਪ ਨ ਹੋਵਈ ਜੇ ਲਾਇ ਰਹਾ ਲਿਵ ਤਾਰ ॥

Akili haiachi kuzurura kwa kubakia kimya hata kwa njia ya kutafakari kila mara.

ਭੁਖਿਆ ਭੁਖ ਨ ਉਤਰੀ ਜੇ ਬੰਨਾ ਪੁਰੀਆ ਭਾਰ ॥

Hata mtu awe na mali kutoka sayari zote, akili haiachi kuwa na tamaa.

ਸਹਸ ਸਿਆਣਪਾ ਲਖ ਹੋਹਿ ਤ ਇਕ ਨ ਚਲੈ ਨਾਲਿ ॥

Mtu anaweza kuwa na busara lakini mwishowe ikawa ni bure.

ਕਿਵ ਸਚਿਆਰਾ ਹੋਈਐ ਕਿਵ ਕੁੜੈ ਤੁਟੈ ਪਾਲਿ ॥

Basi mtu anaweza kuafikia vipi uzima wa milele, na ni vipi mfumo wa imani isiyosahihi unaweza kusimamishwa?

ਹੁਕਮਿ ਰਜਾਈ ਚਲਣਾ ਨਾਨਕ ਲਿਖਿਆ ਨਾਲਿ ॥੧॥

O' Nanak, pazia ya uwongo inaweza tu kutolewa kwa kuishi kulingana na amri ya Mungu, kama vile tu anavyotarajia kutoka kwako.

ਹੁਕਮੀ ਹੋਵਨਿ ਆਕਾਰ ਹੁਕਮੁ ਨ ਕਹਿਆ ਜਾਈ ॥

Kila kitu huwa na mfumo kulingana na matakwa ya Mungu. Matakwa ya Mungu haiwezi kutajwa.

ਹੁਕਮੀ ਹੋਵਨਿ ਜੀਅ ਹੁਕਮਿ ਮਿਲੈ ਵਡਿਆਈ ॥

Nafsi zote zimeumbwa kwa matakwa yake. Utukufu na ukubwa hupatikana kwa matakwa yake.

ਹੁਕਮੀ ਉਤਮੁ ਨੀਚੁ ਹੁਕਮਿ ਲਿਖਿ ਦੁਖ ਸੁਖ ਪਾਈਅਹਿ ॥

Kuna njema na mbovu, yote ni kwa matakwa yake. Maumivu au furaha hupatikana kulingana na matakwa yake, kwa kuzingatia matendo yaliyopita.

ਇਕਨਾ ਹੁਕਮੀ ਬਖਸੀਸ ਇਕਿ ਹੁਕਮੀ ਸਦਾ ਭਵਾਈਅਹਿ ॥

Kwa matakwa yake, watu wengine hubarikiwa na kuwekwa chini ya neema yake, huku wengine wakipotea.

ਹੁਕਮੈ ਅੰਦਰਿ ਸਭੁ ਕੇ ਬਾਹਰਿ ਹੁਕਮ ਨ ਕੋਇ ॥

Kila mwanadamu anatii matakwa yake; hakuna anayeweza kuepuka hilo.

ਨਾਨਕ ਹੁਕਮੈ ਜੇ ਬੁਝੈ ਤ ਹਉਮੈ ਕਰੈ ਨ ਕੋਇ ॥੨॥

O' Nanak, yule ambaye anaelewa matakwa yake hataweza kuwa na ubinafsi.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਤਾਣੁ ਹੋਵੈ ਕਿਸੈ ਤਾਣੁ ॥

Yule mwenye amebarikiwa na nguvu za kiroho kutoka kwa Mungu ndiye anayeweza kusifu ukuu wa mwenye nguvu.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਦਾਤਿ ਜਾਣੈ ਨੀਸਾਣੁ ॥

Wengine huimba juu ya utukufu wake kupitia kwa zawadi zake zilizopokelewa na kuzitambua kama ishara ya neema yake.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਗੁਣ ਵਡਿਆਈਆ ਚਾਰ ॥

Wengine huimba kuhusu ukuu na wema wake.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਵਿਦਿਆ ਵਿਖਮੁ ਵੀਚਾਰੁ ॥

Wengine huimba kumhusu baada ya kumtambua kwa kusoma masomo ya filosofia.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਸਾਜਿ ਕਰੇ ਤਨੁ ਖੇਹ ॥

Wengine huimba kuhusu nguvu zake za kuumba na kuharibu.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਜੀਅ ਲੈ ਫਿਰਿ ਦੇਹ ॥

Wengine huimba kuwa huyachukua maisha na kuyarejesha tena.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਜਾਪੈ ਦਿਸੈ ਦੂਰਿ ॥

Wengine huimba kuwa yeye huonekana mbali sana.

ਗਾਵੈ ਕੇ ਵੇਖੈ ਹਾਦਰਾ ਹਦੂਰਿ ॥

Wengine huimba sifa za Mungu wakimwona kila mahali.

ਕਥਨਾ ਕਥੀ ਨ ਆਵੈ ਤੋਟਿ ॥

Wengi hujaribu kueleza fadhila za Mungu, lakini fadhila zake hazina mwisho.

ਕਥਿ ਕਥਿ ਕਥੀ ਕੋਟੀ ਕੋਟਿ ਕੋਟਿ ॥

Ingawa mamilioni wamejaribu kueleza fadhila zake mamilioni ya nyakati.

ਦੇਦਾ ਦੇ ਲੈਦੇ ਬਕਿ ਪਾਹਿ ॥

Mfadhili Mungu anaendelea kutoa, na wale wanaopokea huchoka kupokea.

ਜੁਗਾ ਜੁਗੰਤਰਿ ਖਾਹੀ ਖਾਹਿ ॥

Viumbe vyote vimekuwa vikitumia vipawa vyake katika enzi zote.

ਹੁਕਮੀ ਹੁਕਮੁ ਚਲਾਏ ਰਾਹੁ ॥

Kwa amri yake, Mwenyezi Mungu, jemadari mkuu, anauendesha ulimwengu kwa njia maalum.

ਨਾਨਕ ਵਿਗਸੈ ਵੇਪਰਵਾਹੁ ॥੩॥

O' Nanak, Mungu siku zote hana wasiwas i na mwenye furaha.

ਸਾਚਾ ਸਾਹਿਬੁ ਸਾਚੁ ਨਾਇ ਭਾਖਿਆ ਭਾਉ ਅਪਾਰੁ ॥

Mungu ni wa milele na haki yake ni ya milele, lughya yake ni upendo na hana kikomo.

ਆਖਹਿ ਮੰਗਹਿ ਦੇਹਿ ਦੇਹਿ ਦਾਤਿ ਕਰੇ ਦਾਤਾਰੁ ॥

Tunamuomba zaidi na zaidi na mpendwa Mungu anaendelea kutoa.

ਫੇਰਿ ਕਿ ਅਗੈ ਰਖੀਐ ਜਿਤੁ ਦਿਸੈ ਦਰਬਾਰੁ ॥

Kisha tumtolee nini ili tuweze kuibua uwepo wake

ਮੁਰੌਂ ਕਿ ਬੋਲਣੁ ਬੋਲੀਐ ਜਿਤੁ ਸੁਣਿ ਧਰੇ ਪਿਆਰੁ ॥

Ni maneno gani tunaweza kusema ili kuamsha upendo Wake?

ਅੰਮ੍ਰਿਤ ਵੇਲਾ ਸਚੁ ਨਾਉ ਵੱਡਿਆਈ ਵੀਚਾਰੁ ॥

Katika saa za ambrose kabla ya mapambazuko, soma Jina la Kweli, na tafakari fadhila Zake tukufu.

ਕਰਮੀ ਆਵੈ ਕਪੜਾ ਨਦਰੀ ਮੇਖੁ ਦੁਆਰੁ ॥

Mwili wa mwanadamu unapatikana kwa matendo mema lakini ukombozi kutoka kwa maovu unapatikana kwa neema yake.

ਨਾਨਕ ਏਵੈ ਜਾਣੀਐ ਸਭੁ ਆਪੇ ਸਚਿਆਰੁ ॥੪॥

O' Nanak, kwa njia hii tunatambua kwamba Mungu ni wa milele, anaenea na ni kila kitu peke yake.

ਬਾਪਿਆ ਨ ਜਾਇ ਕੀਤਾ ਨ ਹੋਇ ॥

Hawezi kuanzishwa (kufungiwa), Hawezi kuumbwa.

ਆਪੇ ਆਪਿ ਨਿਰੰਜਨ ਸੋਇ ॥

Mungu asiye safi alitokea peke yake.

ਜਿਨਿ ਸੇਵਿਆ ਤਿਨਿ ਪਾਇਆ ਮਾਨੁ ॥

Mtu aliymkumbuka kwa kujitoa kwa upendo, ali pokea heshima.

ਨਾਨਕ ਗਾਵੀਐ ਗੁਣੀ ਨਿਧਾਨੁ ॥

O' Nanak, tuimbe sifa za Mungu, hazina ya wema.

ਗਾਵੀਐ ਸੁਣੀਐ ਮਨਿ ਰਖੀਐ ਭਾਉ ॥

Hebu tuimbe na kusikiliza sifa zake, na tuweke upendo wake moyoni mwetu.

ਦੁਖੁ ਪਰਹਰਿ ਸੁਖੁ ਘਰਿ ਲੈ ਜਾਇ ॥

Mtu anayefanya hivi, huondoa huzuni yake na kupata amani ya ndani moyoni mwake.

ਗੁਰਮੁਖਿ ਨਾਦੰ ਗੁਰਮੁਖਿ ਵੇਦੰ ਗੁਰਮੁਖਿ ਰਹਿਆ ਸਮਾਈ ॥

Kupitia Guru tunapata uzoefu wa neno la Mungu, kupitia Guru tunapata ujuzi wa kimungu na kupitia Guru nimetambua kwamba Mungu anaenea.

ਗੁਰੁ ਈਸਰੁ ਗੁਰੁ ਗੋਰਖੁ ਬਰਮਾ ਗੁਰੁ ਪਾਰਬਤੀ ਮਾਈ ॥

Kwa sisi, Guru mwenyewe ni Lord Shiva, Vishnu, Brahma na Parbati. .

ਜੇ ਹਉ ਜਾਣਾ ਆਖਾ ਨਾਹੀ ਕਹਣਾ ਕਥਨੁ ਨ ਜਾਈ ॥

Hata nikitambua Mungu, sitaweza kumaliza kwa sababu hawezu kuelezewa kwa maneno.

ਗੁਰਾ ਇਕ ਦੇਹਿ ਬੁਝਾਈ ॥

Ewe Guru wangu, tafadhali nibariki kwa ufahamu huu kwamba:

ਸਭਨਾ ਜੀਆ ਕਾ ਇਕੁ ਦਾਤਾ ਸੇ ਮੈ ਵਿਸਰਿ ਨ ਜਾਈ ॥੫॥

Huenda usimsahau Mungu, mpaji pekee wa viumbe vyote vilivyo hai.

ਤੀਰਥਿ ਨਾਵਾ ਜੇ ਤਿਸੁ ਭਾਵਾ ਵਿਣੁ ਭਾਣੇ ਕਿ ਨਾਇ ਕਰੀ ॥

Nitaoga kwenye maeneo ya hijja ikiwa tu itampendeza Mungu; bila kumpendeza Mungu, kuna faida gani kuoga kiibada kama hicho?

ਜੇਤੀ ਸਿਰਠਿ ਉਪਾਈ ਵੇਖਾ ਵਿਣੁ ਕਰਮਾ ਕਿ ਮਿਲੈ ਲਈ ॥

Ninapoutazama ulimwengu mzima ulioumbwa Naye, (nimetambua kwamba) hakuna kitu kinacho weza kupatikana bila baraka zake.

ਮਤਿ ਵਿਚਿ ਰਤਨ ਜਵਾਹਰ ਮਾਣਿਕ ਜੇ ਇਕ ਗੁਰ ਕੀ ਸਿਖ ਸੁਣੀ ॥

Akili inakuwa tajiri na maarifa ya kimungu yenge thamani wakati mtu anasikiliza mafundisho ya Guru hata mara moja.

ਗੁਰਾ ਇਕ ਦੇਹਿ ਬੁਝਾਈ ॥

Ewe Guru wangu, naomba unibariki kwa ufahamu huu kwamba;

ਸਭਨਾ ਜੀਆ ਕਾ ਇਕੁ ਦਾਤਾ ਸੈ ਮੈ ਵਿਸਾਰਿ ਨ ਜਾਈ ॥੬॥

Huenda sitamsahau Mungu, mpaji pekee wa viumbe vyote vilivyo hai.

ਜੇ ਜੁਗ ਚਾਰੇ ਆਰਜਾ ਹੋਰ ਦਸੂਣੀ ਹੋਏਂਦਿ ॥

hata kama mtu anaishi katika enzi zote nne, au hata mara kumi zaidi,

ਨਵਾ ਖੰਡਾ ਵਿਚਿ ਜਾਣੀਐ ਨਾਲਿ ਚਲੈ ਸਭੁ ਕੋਇ ॥

na hata kama anajulikana duniani kote na kutiiwa na watu wote.

ਚੰਗਾ ਨਾਉ ਰਖਾਇ ਕੈ ਜਸੁ ਕੀਰਤਿ ਜਗਿ ਲੇਇ ॥

ana sifa nzuri na sifa na umaarufu ulimwenguni kote,

ਜੇ ਤਿਸੁ ਨਦਰਿ ਨ ਆਵਈ ਤ ਵਾਤ ਨ ਪੁੱਛੈ ਕੇ ॥

bado hakuna mtu ambaye angemjali mtu huyo bila neema ya Mungu.

ਕੀਟਾ ਅੰਦਰਿ ਕੀਟੁ ਕਰਿ ਦੋਸੀ ਦੋਸੁ ਧਰੇ ॥

Mtu wa namna hii huhesabiwa kuwa duni sana, (kama mdudu duni), na hata wenye dhambi watamdhara.

ਨਾਨਕ ਨਿਰਗੁਣਿ ਗੁਣੁ ਕਰੇ ਗੁਣਵੰਤਿਆ ਗੁਣੁ ਦੇ ॥

Ee Nanak, Mungu anaweza kuwabariki hata watu wasio wema kwa wema, na anaweza kuwapa wema zaidi watu wema.

ਤੇਹਾ ਕੋਇ ਨ ਸੁਝਈ ਜਿ ਤਿਸੁ ਗੁਣੁ ਕੋਇ ਕਰੇ ॥੧॥

Siwezi hata kufikiria mtu mwingine isipokuwa Mungu ambaye anaweza kuweka wema juu ya wasio na wema.

ਸੁਣਿਐ ਸਿਧ ਪੀਰ ਸੁਰਿ ਨਾਬ ॥

Kwa kusikiliza sifa za Mungu hata watu wa kawaida hupata hadhi ya Sidhas (yogis), Marika (viongozi wa kidini wa Kiislamu), miungu, na Naaths (viongozi wa yoga).

ਸੁਣਿਐ ਧਰਤਿ ਧਵਲ ਆਕਾਸ ॥

Kwa kusikiliza Naam (mtu anaelewa fumbo la) dunia, na fahali halisi (au nguvu), ambayo inategemeza dunia na anga.

ਸੁਣਿਐ ਦੀਪ ਲੋਅ ਪਾਤਾਲ ॥

Kwa kusikiliza Naam, mtu anaelewa kwamba Mungu anaenea katika mabara yote, ulimwengu, na maeneo ya chini.

ਸੁਣਿਐ ਪੇਹਿ ਨ ਸਕੈ ਕਾਲੁ ॥

Kwa kusikiliza sifa za Mungu, mtu haogopi kifo.

ਨਾਨਕ ਭਰਤਾ ਸਦਾ ਵਿਗਾਸੁ ॥

O' Nanak, waja wake wako katika furaha na raha milele.

ਸੁਣਿਐ ਦੂਖ ਪਾਪ ਕਾ ਨਾਸੁ ॥੮॥

Kusikiliza sifa za Mungu, huzuni na dhambi zote zinafutwa.

ਸੁਣਿਐ ਈਸਰੁ ਬਰਮਾ ਇੰਦੁ ॥

Kusikiliza Naam, mtu hupata sifa za kimungu kama zile za Shiva, Brahma na Indra.

ਸੁਣਿਐ ਮੁਖਿ ਸਾਲਾਹਣ ਮੰਦੁ ॥

Kwa kusikiliza Naam, hata wenye dhambi wanapata nuru na kuanza kuimba sifa za Mungu.

ਸੁਣਿਐ ਜੋਗ ਜੁਗਤਿ ਤਨਿ ਭੇਦ ॥

Kwa kumsikiliza Naam, mtu anaanza kuelewa siri za kuungana na Mungu, na siri za mwili wa mwanadamu.

ਸੁਣਿਐ ਸਾਸਤ ਸਿਮ੍ਰਿਤਿ ਵੇਦ ॥

Kwa kusikiliza Jina la Mungu, mtu anapata ujuzi wa kiroho unaofafanuliwa katika maandiko matakatifu.

ਨਾਨਕ ਭਗਤਾ ਸਦਾ ਵਿਗਾਸੁ ॥

O' Nanak, waja wa Mungu wako katika raha milele.

ਸੁਣਿਐ ਦੁਖ ਪਾਪ ਕਾ ਨਾਸੁ ॥੯॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, uchungu, huzuni na dhambi zote hufutiliwa mbali.

ਸੁਣਿਐ ਸਤੁ ਸੰਤੋਖੁ ਗਿਆਨੁ ॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, mtu hujua ukweli, hutoshuka na kuwa na maarifa ya kiroho.

ਸੁਣਿਐ ਅਠਸਠਿ ਕਾ ਇਸਨਾਨੁ ॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, mtu huwa mwenye haki.

ਸੁਣਿਐ ਪੜਿ ਪੜਿ ਪਾਵਹਿ ਮਾਨੁ ॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, mtu hupata maarifa ya kiukuu na heshima ya kweli.

ਸੁਣਿਐ ਲਾਗੈ ਸਹਜਿ ਧਿਆਨੁ ॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, akili ya mtu huwa na uwezo wa kutafakari mambo mapya.

ਨਾਨਕ ਭਗਤਾ ਸਦਾ ਵਿਗਾਸੁ ॥

O' Nanak, wafuasi wa Mungu wako katika hali ya furaha na neema milele.

ਸੁਣਿਐ ਦੁਖ ਪਾਪ ਕਾ ਨਾਸੁ ॥੧੦॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, uchungu, huzuni na dhambi zote hufutiliwa mbali.

ਸੁਣਿਐ ਸਰਾ ਗੁਣਾ ਕੇ ਗਾਹ ॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, mtu huwa na wema zaidi.

ਸੁਣਿਐ ਸੇਖ ਪੀਰ ਪਾਤਿਸਾਹ ॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, mtu hupata neema ya kiroho

ਸੁਣਿਐ ਅੰਧੇ ਪਾਵਹਿ ਰਾਹੁ ॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, mtu aliye mdhaifu kiroho huelimika na kufuata mkondo unaofaa.

ਸੁਣਿਐ ਹਾਥ ਹੋਵੈ ਅਸਗਾਹੁ ॥

Ukisikiza, yaliyombali hupatikana kwa urahisi.

ਨਾਨਕ ਭਰਤਾ ਸਦਾ ਵਿਗਾਸੁ ॥

O' Nanak, wafuasi wa Mungu wako katika hali ya furaha na neema milele.

ਸੁਣਿਐ ਦੂਖ ਪਾਪ ਕਾ ਨਾਸੁ ॥੧੧॥

Kwa kusikiza neno la Mungu kwa upendo na kujitolea, uchungu, huzuni na dhambi zote hufutiliwa mbali.

ਮੰਨੇ ਕੀ ਗਤਿ ਕਹੀ ਨ ਜਾਇ ॥

Hali ya kiroho ya akili iliyo na imani kamilifukatika jina la Mungu ni ya juu sanakiasi cha kutoelezwa.

ਜੇ ਕੇ ਕਰੈ ਪਿਛੈ ਪਛਤਾਏ ॥

Yeyote anayejaribu kuelezea atajutia jaribio lake.

ਕਾਗਦਿ ਕਲਮ ਨ ਲਿਖਣਹਾਰੁ ॥ਮੰਨੇ ਕਾ ਬਹਿ ਕਰਨਿ ਵੀਰਾਰੁ ॥

Watu huthamini hali ya kiroho ya aina hiyo yar oho iliyoinuliwa,lakini hakuna yeyote anayeweza kuikamata nakuiandika.

ਐਸਾ ਨਾਮੁ ਨਿਰੰਜਨੁ ਹੋਇ ॥ ਜੇ ਕੇ ਮੰਨਿ ਜਾਣੈ ਮਨਿ ਕੋਇ ॥੧੨॥

Jina la Mungu ni safi kikamilifu. Yule aliye na imani kamilifu na anayeishi kulingana na ushauri wa Guru ndiye anayeweza kupata ladha ya utakaso wake mkuu.

ਮੰਨੈ ਸੁਰਤਿ ਹੋਵੈ ਮਨਿ ਬੁਧਿ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mtu hupata uwezo wa kuyajua mambo bila ugumu wowote, na kupata elimu ya kiroho.

ਮੰਨੈ ਸਗਲ ਭਵਣ ਕੀ ਸੁਧਿ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mtu hupata kuelewa kwa njia ya kiroho kuwa Mungu anapatikana kila mahali.

ਮੰਨੈ ਮੁਹਿ ਚੇਟਾ ਨਾ ਖਾਇ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mtu hawezo kuteseka kutokana na uchungu wa mabaya ya ulimwengu.

ਮੰਨੈ ਜਮ ਕੈ ਸਾਥਿ ਨ ਜਾਇ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mzunguko wa kuzaliwa na kufa humuondokea mtu.

ਐਸਾ ਨਾਮੁ ਨਿਰੰਜਨੁ ਹੋਇ ॥ਜੇ ਕੋ ਮੰਨਿ ਜਾਣੈ ਮਨਿ ਕੋਇ ॥੧੩॥

Jina la Mungu ni safi kikamilifu. Yule aliye na Imani kamilifu na anayeishi kulingga na ushauri wa Guru ndiyе anayeweza kupata ladha ya utakaso wake mkuu.

ਮੰਨੈ ਮਾਰਗਿ ਠਾਕ ਨ ਪਾਇ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mkondo wa kiroho wa waumini hautazuiliwa na chochote.

ਮੰਨੈ ਪਤਿ ਸਿਉ ਪਰਗਟੁ ਜਾਇ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, wale waumini wataondoka duniani katika hali kubwa ya kiroho.

ਮੰਨੈ ਮਗੁ ਨ ਚਲੈ ਪੰਥੁ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mtu hawezo kufuata mkondo wa matambiko ya madhehebu ya kidini.

ਮੰਨੈ ਧਰਮ ਸੇਤੀ ਸਨਬੰਧੁ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, waumini wamejikita katika mkondo wa ukweli na haki.

ਐਸਾ ਨਾਮੁ ਨਿਰੰਜਨੁ ਹੋਇ ॥ਜੇ ਕੋ ਮੰਨਿ ਜਾਣੈ ਮਨਿ ਕੋਇ ॥੧੪॥

Jina la Mungu ni safi kikamilifu. Yule aliye na Imani kamilifu na anayeishi kulingga na ushauri wa Guru ndiyе anayeweza kupata ladha ya utakaso wake mkuu.

ਮੰਨੈ ਪਾਵਹਿ ਮੇਖੁ ਦੁਆਰੁ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mtu anapata ukombozi kutoka kwa mzunguko wa kuzaliwa na kufa.

ਮੰਨੈ ਪਰਵਾਰੈ ਸਾਧਾਰੁ ॥

Kwa kuwa na imani kamilifu katika Mungu, mtu anavihuisha viungo vyake vyote via hisia katika kutafakari kuhusu neno la Mungu.

ਮੰਨੈ ਤਰੈ ਤਾਰੇ ਗੁਰੁ ਸਿਖ ॥

Kwa kuwa na imani kwa Mungu, mtu hupita juu ya bahari ya kilimwengu iliyojaa mabaya, na kusaidia wafuasi wa Guru kujikomboa kutoka kwa mzunguko wa kuzaliwa na kufa.

ਮੰਨੈ ਨਾਨਕ ਭਵਹਿ ਨ ਭਿਖ ॥

Kwa kuwa na imani katika Mungu, O' Nanak, mtu hawezo kuzurura kujitosheleza kutoka kwa mtu yeyote.

ਐਸਾ ਨਾਮੁ ਨਿਰੰਜਨੁ ਹੋਏ ॥ ਜੇ ਕੇ ਮੰਨਿ ਜਾਣੈ ਮਨਿ ਕੋਇ ॥੧੫॥

Jina la Mungu ni safi kikamilifu. Yule aliye na Imani kamilifu na anayeishi kulingana na ushauri wa Guru ndiye anayeweza kupata ladha ya utakaso wake mkuu.

ਪੰਚ ਪਰਵਾਣ ਪੰਚ ਪਰਧਾਨੁ ॥ ਪੰਚੇ ਪਾਵਹਿ ਦਰਗਹਿ ਮਾਨੁ ॥

Waliojikita kwa jina lake Mungu wamebarikiwa ili kuinuliwa kiroho na kuheshimiwa.

ਪੰਚੇ ਸੋਹਹਿ ਦਰਿ ਰਾਜਾਨੁ ॥ ਪੰਚਾ ਕਾ ਗੁਰੁ ਏਕੁ ਧਿਆਨੁ ॥

Miyo hiyo iliyojikita katika jina la Mungu ni teule na lengo lao liko katika neno kuu la Mungu.

ਜੇ ਕੇ ਕਰੈ ਕਰੈ ਵੀਚਾਰੁ ॥ ਕਰਤੇ ਕੈ ਕਰਣੈ ਨਾਹੀ ਸੁਮਾਰੁ ॥

Ikiwa mtu atajaribu kueleza jinsi Mungu alivyo, itakuwa wazi kuwa ni vigumu kueleza jinsi alivyo kwa kuwa hakuna kikomo katika uumbaji wake.

ਧੌਲੁ ਧਰਮੁ ਦਇਆ ਕਾ ਪੂਤੁ ॥

Haki ama dini ni kizazi cha rehema. Nguvu za rehema hii ndio inayodhaniwa kuwa fahali anayeshikilia dunia.

ਸੰਤੋਖ ਥਾਪਿ ਰਖਿਆ ਜਿਨਿ ਸੂਤਿ ॥

Kwa kawaida, usawa unadumishwa na haki, rehema na kuridhika.

Fadhila(wema) hizi tatu ndizo zinazouweka ulimwengu katika mpangilio mwema kama shanga katika uzi.

ਜੇ ਕੇ ਬੁਝੈ ਹੋਵੈ ਸਚਿਆਰੁ ॥ ਧਵਲੈ ਉਪਰਿ ਕੇਤਾ ਭਾਰੁ ॥

Anayeelewa usawa wa fadhila hizi anakua wa kweli. Ni sharia kuu ndizo zinaweka ulimwengu katika usawa, wala sio fahali kama ilivyo katika dini ya kitambo ya Kihindi.

ਧਰਤੀ ਹੋਰੁ ਪਰੈ ਹੋਰੁ ਹੋਰੁ ॥ ਤਿਸ ਤੇ ਭਾਰੁ ਤਲੈ ਕਵਣ ਜੋਰੁ ॥

Kuna dunia nyingi zaidi ya dunia hii. Na mbele ya hiso,kuna nyingi zaidi.Ni nguvu gani inazishikilia pamoja na uzito wao?

ਜੀਅ ਜਾਤਿ ਰੰਗਾ ਕੇ ਨਾਵ ॥ ਸਭਨਾ ਲਿਖਿਆ ਵੁੜੀ ਕਲਾਮ ॥

Majina na rangi ya viumbe mbalimbali vinaviokaribiana yaliandikwa kwa kalamu ya milele ya Mungu.

ਏਹੁ ਲੇਖਾ ਲਿਖਿ ਜਾਣੈ ਕੋਇ ॥ ਲੇਖਾ ਲਿਖਿਆ ਕੇਤਾ ਹੋਇ ॥

Ni vipi mtu anaweza kuandika masimulizi kuhusu haya? Yataku masimulizi yasiyokuwa na mwisho!

ਕੇਤਾ ਤਾਣੁ ਸੁਆਲਿਹੁ ਰੂਪੁ ॥ ਕੇਤੀ ਦਾਤਿ ਜਾਣੈ ਕੌਣੁ ਕੂਡੁ ॥

Nguvu yake ni kubwa! Uzuri wake wa kusisimua! Zawadi nzuri! Ni nani anaweza kujua kipimo chao?

ਕੀਤਾ ਪਸਾਉ ਏਕੇ ਕਵਾਉ ॥ ਤਿਸ ਤੇ ਹੋਏ ਲਖ ਦਰੀਆਉ ॥

Uliumba ukubwa wa ulimwengu kwa neno moja! Na mamia ya maelfu ya viumbe wakaibuka.

ਕੁਦਰਤਿ ਕਵਣ ਕਹਾ ਵੀਚਾਰੁ ॥ ਵਾਰਿਆ ਨ ਜਾਵਾ ਏਕ ਵਾਰ ॥

Hata sina nguvu ya kuanza kuelezea uumbaji wako; sina chochote cha kutoa kinachostahili ukuu wako, hata maisha yangu hayatoshi.

ਜੋ ਤੁਧੁ ਭਾਵੈ ਸਾਈ ਭਲੀ ਕਾਰ ॥ ਤੂ ਸਦਾ ਸਲਾਮਤਿ ਨਿਰੰਕਾਰ ॥੧੯॥

Chochote kinachokufarisha wewe Mungu, ni bora kwa kila mtu.Wewe pekee ndiye wa milele na hauna umbo.

असंख जप असंख भाउ ॥ असंख पूजा असंख उप ताउ ॥

Wanaotafakari juu ya jina lako kwa upendo hawahesabiki. Wanaokuabudu na kufanya mambo mengi magumu hawahesabiki.

असंख गरंघ मुखि वेद पाठ ॥ असंख जेग मनि रहहि उदास ॥

Maandiko na ibada ukariri wa ibada za Vedas hazihesabiki. Yogis ambao akili zao zimebaki kuwa mbali na dunia hawahesabiki.

असंख भगत गुण गिआन वीचार ॥

Wahumini wengi wasiohesabika wametafakari wema na hekima ya Mwenyezi Mungu.

असंख सती असंख दातार ॥

Kuna watu watakatifu na watu wenye kusaidia wengine, hawahesabiki.

असंख सुर मुह भख सार ॥

Kuna mashujaa wengi wa kiroho ambao hushambuliwa vikali katika uwanja wa vita vyta kimaisha, hawahesabiki.

असंख मेनि लिव लाइ तार ॥

Kuna watu wengi wasiohesabika walijitolea na wameunganishwa na Mwenyezi Mungu kwa nia moja tu, ya kujitolea.

बुदरति कवण कहा वीचारु ॥

Jinsi nilivyo bila nguvu, nitawezaje kuelezea uumbaji wako mkubwa.

वारिआ न जाहा एक वार ॥

Sina chochote cha kutoa kinachostahili ukuu wako, hata maisha yangu hayatoshi.

जे डुय भावै साई भली कार ॥ डु सदा सलामति निर्दकार ॥१७॥

Chochote kinachokufarisha wewe, ni bora kwa kila mtu. Wewe pekee ndiye wa milele na hauna umbo.

असंख मूरख अंय घोर ॥

Wapumbavu waliopofushwa kwa ujinga ni wengi, hawahesabiki

ਅਸੰਖ ਚੇਰ ਹਰਾਮਖੇਰ ॥

Wezi na wafujaji ni wengi, hawahesabiki

ਅਸੰਖ ਅਮਰ ਕਰਿ ਜਾਹਿ ਜੋਰ ॥

Wanaolazimisha matakwa yao ni wengi, hawahesabiki.

ਅਸੰਖ ਗਲਵਦ਼ ਹਤਿਆ ਕਮਾਹਿ ॥

Wanyongaji na wauaji wasio na huruma ni wengi, hawahesabiki

ਅਸੰਖ ਪਾਪੀ ਪਾਪੁ ਕਰਿ ਜਾਹਿ ॥

Wenye dhambi wanaoendelea kutenda dhambi ni wengi, hawahesabiki.

ਅਸੰਖ ਕੂੜਿਆਰ ਕੂੜੇ ਫਿਰਾਹਿ ॥

Waongo waliopotelea katika uwongo wao ni wengi, hawahesabiki.

ਅਸੰਖ ਮਲੇਛ ਮਲੁ ਭਖਿ ਖਾਹਿ ॥

Waovu wanaonawiri kwa mienendo yao miovu ni wengi, hawahesabiki.

ਅਸੰਖ ਨਿੰਦਕ ਸਿਰਿ ਕਰਹਿ ਭਾਰੁ ॥

Wasemaji uongo wanaoendelea kutenda dhambi kwa kuongea mabaya kwa wengine ni wengi, hawahesabiki.

ਨਾਨਕੁ ਨੀਚੁ ਕਰੈ ਵੀਚਾਰੁ ॥

Katika beti za hapo awali, Nanak anaelezea kuhusu watu wa hali ya chini.

ਵਾਰਿਆ ਨ ਜਾਵਾ ਏਕ ਵਾਰ ॥

Sina chochote cha kutoa kinachostahili ukuu wako, hata maisha yangu hayatoshi.

ਜੇ ਤੁਧੁ ਭਾਵੈ ਸਾਈ ਭਲੀ ਕਾਰ ॥ ਤੂ ਸਦਾ ਸਲਾਮਤਿ ਨਿਰੰਕਾਰ ॥੧੮॥

Chochote kinachokufarisha wewe, ni bora kwa kila mtu. Wewe pekee ndiye wa milele na hauna umbo.

ਅਸੰਖ ਨਾਵ ਅਸੰਖ ਥਾਵ ॥

Majina ya vitu ulivyoumba hayahesabiki, na makao yao hayahesabiki.

ਅਰੰਮ ਅਰੰਮ ਅਸੰਖ ਲੋਅ ॥

Kuna dunia nyingi zisizoweza kufikiwa na kukaribiwa.

असंख कहरि सिरि भारु होइ ॥

Hata neno 'kutohesabika' haliwezi kuwasilisha hali ya uumbaji wake usiokuwa na mwisho.

अखरी नामु अखरी सालाह ॥

Ni kwa kutumia maneno, kwamba jina lake linaweza kukaririwa; ni kwa kutumia maneno, kwamba sifa zake zinaweza kuimbwa.

अखरी गिआनु गीत गुण गाह ॥

Elimu ya kiukuu hupatikana kupitia kwa maneno. Sifa zake huimbwa na wema wake kujilikana.

अखरी लिख्ण बैल्ण बाटि ॥

Lugha iliyoandikwa na ile ya kuzungumzwa inaweza tu kuonyeshwa kupitia kwa maneno.

अखरा सिरि संजेगु व्याटि ॥

Hatima ya mtu huelezwa kwa kutumia maneno.

जिनि एहि लिखे तिसु सिरि नाहि ॥

Yeye {Mungu} aliyeandika hatima ya kila mtu, hana mwisho.

जिव छुरमाए तिव तिव पाहि ॥

Anavyoamuru ndivyo tupokeavyo

जेता कीता उत्ता नाउ ॥ विणु नाहै नाही के थाउ ॥

Ulimwengu ni dhihirisho la jina lako. Hakuna mahali ambapo Mungu hapatikani.

कुसरति कवण कहा वीसारु ॥ वारिआ न जावा एक वार ॥

Nawezaje kuelezea nguvu zako bunifu? Hata siwezi nikawa dhabihu kwako.

जे डुपु भाहै साई भली कार ॥ डु मदा मलामति निर्कार ॥१८॥

Chochote kinachokufarisha wewe Mungu, ni bora kwa kila mtu. Wewe pekee ndiye wa milele na hauna umbo.

बरीऐ रघु पैरु उनु देह ॥ पाणी येतै उउरसु खेह ॥

Mikono, miguu na mwili ikichafuka, maji inaweza kuondoa uchafu.

ਮੁਤ ਪਲੀਤੀ ਕਪੜ੍ਹ ਹੋਇ ॥ ਦੇ ਸਾਬੂਣ੍ਹ ਲਈਐ ਓਹੁ ਧੋਇ ॥

Sabuni inaweza kutumika kuosha nguo zinapochafuliwakwa mkojo na kadhalika.

ਭਰੀਐ ਮਤਿ ਪਾਪਾ ਕੈ ਸੰਗਿ ॥ ਓਹੁ ਧੋਪੈ ਨਾਵੈ ਕੈ ਰੰਗਿ ॥

Lakini akili inapochafuliwa kwa fikira mbovu na dhambi, inaweza kusafishwa tu kwa kukariri na upendo kwa Naam (neno la Mungu)

ਪੁੰਨੀ ਪਾਪੀ ਆਖਣੁ ਨਾਹਿ ॥ ਕਰਿ ਕਰਿ ਕਰਣਾ ਲਿਖਿ ਲੈ ਜਾਹੁ ॥

Waadili au wenyе dhambi sio majina tu. Tunakua watu wema (waadili) ama wenyе dhambi kulingana namatendo tunayotenda. Tunayabeba matendo hayo hadi kwenye maisha yajayo.

ਆਪੇ ਬੀਜਿ ਆਪੇ ਹੀ ਖਾਹੁ ॥ ਨਾਨਕ ਹੁਕਮੀ ਆਵਹੁ ਜਾਹੁ ॥੨੦॥

Utavuna unachokipanda. Zawadi na adhabu ni matunda ya matendo yetu. O' Nanak. kulingana na sharia zake kuu, unakuja na kuondokaduniani kulingana na matendo yako.

ਤੀਰਥੁ ਤਪੁ ਦਇਆ ਦਤੁ ਦਾਨੁ ॥ ਜੇ ਕੇ ਪਾਵੈ ਤਿਲ ਕਾ ਮਾਨੁ ॥

Hija, mambo magumu, rehema na hisani huleta neema kidogo sana.

ਸੁਣਿਆ ਮੰਨਿਆ ਮਨਿ ਕੀਤਾ ਭਾਉ ॥ ਅੰਤਰਗਤਿ ਤੀਰਥਿ ਮਲਿ ਨਾਉ ॥

Yeyote yule anayesikiza Naam (neno la Mungu) kwa kwakujitolea kikamilifu na upendo katika moyo wake, anafanya hija ya kweli kwa kujiosha nafsi.

ਸਭਿ ਗੁਣ ਤੇਰੇ ਮੈ ਨਾਹੀ ਕੋਇ ॥ ਵਿਣੁ ਗੁਣ ਕੀਤੇ ਭਗਤਿ ਨ ਹੋਇ ॥

Inawezekana kupata fadhila (wema) kwa kuachana na ego na kukariri Naam (neno la Mungu). Fadhil azote ni katika kukusifu, mwenye nguvu. Bila Fadhila, hakuwezi kuwepo na ibada ya kujitolea.

ਸੁਆਸਤਿ ਆਖਿ ਬਾਣੀ ਬਰਮਾਉ ॥ ਸਤਿ ਸੁਹਾਣੁ ਸਦਾ ਮਨਿ ਚਾਉ ॥

Nakuinamia wewe muumba wa Maya na muumbaji wa neno kuu. Unaishi milele na unapendeza, na furaha ya kindani isiyo na kikomo.

ਕਵਣੁ ਸੁ ਵੇਲਾ ਵਖਤੁ ਕਵਣੁ ਕਵਣੁ ਥਿਤਿ ਕਵਣੁ ਵਾਰੁ ॥ ਕਵਣਿ ਸਿ ਰੁਤੀ ਮਾਹੁ ਕਵਣੁ ਜਿਤੁ ਹੋਆ ਆਕਾਰੁ ॥

Saa hiyo ilikua ipi, na wakati huo ulikua upi? Ilikua siku gani? Na ilikua tarehe gani? Yalikua majira gani, na ulikua mwezi upi, dunia ilipoumbwa?

ਵੇਲ ਨ ਪਾਈਆ ਪੰਡਤੀ ਜਿ ਹੋਵੈ ਲੇਖੁ ਪੁਰਾਣੁ ॥

Pandits (wasomi wa dini ya kihindi) hawakujua wakati dunia ilipoumbwa, la sivyo wangekua wameandika katika Puranas (vitabu vyatika kihindi).

ਵਖਤੁ ਨ ਪਾਇਓ ਕਾਦੀਆ ਜਿ ਲਿਖਨਿ ਲੇਖੁ ਕੁਰਾਣੁ ॥

Hata Qadi (wasomi wa dini ya kiislamu) hawakujia, la sivyo wangekua wameandika katika Quran.

ਬਿਤਿ ਵਾਰੁ ਨਾ ਜੋਗੀ ਜਾਣੈ ਰੁਤਿ ਮਾਹੁ ਨਾ ਕੋਈ ॥ ਜਾ ਕਰਤਾ ਸਿਰਠੀ ਕਉ ਸਾਜੇ ਆਪੇ ਜਾਣੈ ਸੋਈ ॥

Yogis hawakujua siku, tarehe, mwezi au majira ambapo dunia iliumbwa. Ni Mungu muumbaji pekee anayejua wakati alipoumba dunia.

ਕਿਵ ਕਰਿ ਆਖਾ ਕਿਵ ਸਾਲਾਹੀ ਕਿਉ ਵਰਨੀ ਕਿਵ ਜਾਣਾ

Nawezaje kuzungumzia ukubwa wake? Nawezaje kumsifu? Nawezaje kuelezea fadhila(wema) ake? Nawezaje kumjua?

ਨਾਨਕ ਆਖਣਿ ਸਭੁ ਕੇ ਆਖੈ ਇਕ ਦੂ ਇਕੁ ਸਿਆਣਾ ॥

O' Nanak, kila mtu anamzungumzia na kujifanya kuwa mwerevu zaidi kuliko wengine.

ਵਡਾ ਸਾਹਿਬੁ ਵਡੀ ਨਾਈ ਕੀਤਾ ਜਾ ਕਾ ਹੋਵੈ ॥

Ukuu ni wa aliyemkuu. Jina lake ni kuu. Kila kitu hufanyikakulingana na matakwa yake.

ਨਾਨਕ ਜੇ ਕੇ ਆਪੈਂ ਜਾਣੈ ਅਗੈ ਗਇਆ ਨ ਸੋਹੈ ॥੨੧॥

O' Nanak, yule anayedai kumjua Mungu asiyejulikana kikamilifu hawezu kustahili neema zake.

ਪਾਤਾਲਾ ਪਾਤਾਲ ਲਖ ਆਗਾਸਾ ਆਗਾਸ ॥

Kuna dunia za jahanamu chini ya dunia za jahanamu, na mamia ya maelfu ya dunia za juu mbinguni.

ਓੜਕ ਓੜਕ ਭਾਲਿ ਥਕੇ ਵੇਦ ਕਰਨਿ ਇਕ ਵਾਤ ॥

Vedas wanasema kuwa wasomi wamechoka wakijaribu kupata mipaka ya uumbaji wake Mungu.

ਸਹਸ ਅਠਾਰਹ ਕਹਨਿ ਕਤੇਬਾ ਅਸੁਲੂ ਇਕੁ ਧਾਤੁ ॥

Maandiko yanasema kuwa kuna dunia 18,000. Ki ukweli, ni nyingi mno, n azote zina asili moja, Mungu mwenyewe.

ਲੇਖਾ ਹੋਇ ਤ ਲਿਖੀਐ ਲੇਖੈ ਹੋਇ ਵਿਣਾਸੁ ॥

Haiwezekani kamwe kuhesabu uumbaji wa Mungu usio na kikomo. Hakuna hata idadi inayoweza kutumiwa kuelezea.

ਨਾਨਕ ਵਡਾ ਆਖੀਐ ਆਪੇ ਜਾਣੈ ਆਪੁ ॥੨੨॥

O' Nanak, Mungu ni mkuu, na anajua alivyo mkuu.

ਸਾਲਾਹੀ ਸਾਲਾਹਿ ਏਤੀ ਸੁਰਤਿ ਨ ਪਾਈਆ ॥

Wale wanaomsifu Mungu anayependeza na kuungana naye lakini hawawezi kuchanganua ukuu wa utukufu wake.

ਨਦੀਆ ਅਤੈ ਵਾਹ ਪਵਹਿ ਸਮੁੰਦਿ ਨ ਜਾਣੀਅਹਿ ॥

Ni kama vijito na mito inayoelekea kwenye bahari na kuungana nayo na haiwezi kujua ukubwa wa bahari hiyo.

ਸਮੁੰਦ ਸਾਹ ਸੁਲਤਾਨ ਗਿਰਹਾ ਸੇਤੀ ਮਾਲੁ ਧਨੁ ॥ ਕੀੜੀ ਤੁਲਿ ਨ ਹੋਵਨੀ ਜੇ ਤਿਸੁ ਮਨਹੁ ਨ ਵੀਸਰਹਿ ॥੨੩॥

Hata wafalme na watawala wenye mali na utajiri mkubwa hawawezi kutoshana na mtu maskini hohe hahe asiyemsahau Mungu.

ਅੰਤੁ ਨ ਸਿਫਤੀ ਕਹਣਿ ਨ ਅੰਤੁ ॥

Fadhila(wema) za Mungu, pamoja na maelezo ya hiso fadhila, hayana mwisho.

ਅੰਤੁ ਨ ਕਰਣੈ ਦੇਣਿ ਨ ਅੰਤੁ ॥

Hakuna mwisho kwa uumbaji wake; hakuna mwisho kwa zawadi zake.

ਅੰਤੁ ਨ ਵੇਖਣਿ ਸੁਣਣਿ ਨ ਅੰਤੁ ॥

Hakuna mwisho kwa viumbi wake, wala hakuna mwisho kwa sauti ya maubile yake hata kama itajaribiwa kwa muda mrefu.

ਅੰਤੁ ਨ ਜਾਪੈ ਕਿਆ ਮਨਿ ਮੰਤੁ ॥

Ni vigumu kujua kikomo cha miundo yake.

ਅੰਤੁ ਨ ਜਾਪੈ ਕੀਤਾ ਆਕਾਰੁ ॥ ਅੰਤੁ ਨ ਜਾਪੈ ਪਾਰਾਵਾਰੁ ॥

Mipaka ya dunia iliyoundwa haiwezi kutambuliwa.

ਅੰਤ ਕਾਰਣਿ ਕੇਤੇ ਬਿਲਲਾਹਿ ॥ ਤਾ ਕੇ ਅੰਤ ਨ ਪਾਏ ਜਾਹਿ ॥

Watu wengi wanajitahidi kujua mipaka yake, lakini haipatikani.

ਏਹੁ ਅੰਤੁ ਨ ਜਾਣੈ ਕੋਇ ॥ ਬਹੁਤਾ ਕਹੀਐ ਬਹੁਤਾ ਹੋਇ ॥

Hakuna anayeweza kujua hizi mipaka, na jinsi inavyoongelewa, ndivyo inavyozidi kuongelewa.

ਵਡਾ ਸਾਹਿਬੁ ਉਚਾ ਥਾਉ ॥ ਉਚੇ ਉਪਰਿ ਉਚਾ ਨਾਉ ॥

Ukuu ni wa aliyemkuu na kutokuwa na kikomo ni makao yake ya mbinguni. Aliye juu zaidi ndilo jina lake.

ਏਵੱਡੁ ਉਚਾ ਹੋਵੈ ਕੋਇ ॥ ਤਿਸੁ ਉਚੇ ਕਉ ਜਾਣੈ ਸੋਇ ॥

Ni mtu mkuu kama Mungu mwenyewe mwenye uwezo wa kujua hali ya Mungu wa juu na iliyoinuliwa.

ਜੇਵੱਡੁ ਆਪਿ ਜਾਣੈ ਆਪਿ ਆਪਿ ॥

Ni Mungu mwenyewe ndiye anayejua alivyo mkuu.

ਨਾਨਕ ਨਦਰੀ ਕਰਮੀ ਦਾਤਿ ॥੨੪॥

O' Nanak, kwa neema zake, anapeana baraka zake.

ਬਹੁਤਾ ਕਰਮੁ ਲਿਖਿਆ ਨਾ ਜਾਇ ॥

Baraka zake ni nyingi kiasi cha kutoweza kuhesabika.

ਵਡਾ ਦਾਤਾ ਤਿਲੁ ਨ ਤਮਾਇ ॥

Mpeanaji mkuu anaamini tu katika kupeana, na hana choyo hata kidogo.

ਕੇਤੇ ਮੰਗਹਿ ਜੋਧ ਅਪਾਰ ॥

Mashujaa wengi wanaomba kutoka kwa Mungu asiye na mwisho.

ਕੇਤਿਆ ਗਣਤ ਨਹੀ ਵੀਚਾਰੁ ॥

Ni wengi wanaotafakari na kukaa juu yake, hawahesabiki.

ਕੇਤੇ ਖਪਿ ਤੁਟਹਿ ਵੇਕਾਰ ॥

Wengi wanajiingiza katika matendo mabaya na kuaga kwa sababu ya wasiwasi.

ਕੇਤੇ ਲੈ ਲੈ ਮੁਕਰੁ ਪਾਹਿ ॥

Wengi wanazidi kupocea zawadi zake Mungu lakini wanakana kuzipata (kwa kutomshukuru).

ਕੇਤੇ ਮੂਰਖ ਖਾਹੀ ਖਾਹਿ ॥

Wapumbavu wengi wanaendelea kupocea, lakini wanashahau anayepeana.

ਕੋਤਿਆ ਦੂਖ ਭੁਖ ਸਦ ਮਾਰ ॥

Ni wengi ambaو wataendelea kuvumilia mafadhaiko, kunyimwa na kunyanyaswa kila mara.

ਏਹਿ ਭਿ ਦਾਤਿ ਤੇਰੀ ਦਾਤਾਰ ॥

Haya mateso ni baraka zako pia, mpeanaji mkuu (kwa sababu yanaturudisha kwako kwa kupata fadhila zako).

ਬੰਦਿ ਖਲਾਸੀ ਭਾਣੈ ਹੋਇ ॥ ਹੋਰੁ ਆਖਿ ਨ ਸਕੈ ਕੋਇ ॥

Uhuru kutoka kwa ego na mambo ya dunia inaafikiwa tu kwa kukubali matakwa yako. Hakuna mwingine aliye na usemi juu ya hilo.

ਜੇ ਕੇ ਖਾਇਕੁ ਆਖਣਿ ਪਾਇ ॥ ਓਹੁ ਜਾਣੈ ਜੇਤੀਆ ਮੁਹਿ ਖਾਇ ॥

Ikiwa mtu mpumbavu atapendekeza njia yoyote ile zaidi ya kukubali matakwa ya Mungu keupuka ushirika na Maya, atakabiliwa na athari za upumbavu wake.

ਆਪੇ ਜਾਣੈ ਆਪੇ ਦੇਇ ॥ ਆਖਹਿ ਸਿ ਭਿ ਕੇਈ ਕੋਇ ॥

Ni ye ye mwenyewe anajua mahitaji yetu na anazidi kuyatimiza. Ni wachache wanaoshukuru kwa hili.

ਜਿਸ ਨੇ ਬਖਸੇ ਸਿਫਤਿ ਸਾਲਾਹ ॥ ਨਾਨਕ ਪਾਤਿਸਾਹੀ ਪਾਤਿਸਾਹੁ ॥੨੫॥

O' Nanak, aliyebarikiwa na hazina ya kumsifu Mungu, ndiye mtu mwenye utajiri mkubwa wa kiroho duniani.

ਅਮੁਲ ਗੁਣ ਅਮੁਲ ਵਾਪਾਰ ॥

Fadhila (wema) za Mungu hazina bei. Juhudi ya kupata fadhila hiso hazina bei.

ਅਮੁਲ ਵਾਪਾਰੀਏ ਅਮੁਲ ਭੰਡਾਰ ॥

Wale wanaopata fadhila(wema) zake hawana bei. Hazina zake hazina bei.

ਅਮੁਲ ਆਵਹਿ ਅਮੁਲ ਲੈ ਜਾਹਿ ॥

Wanaokuja duniani na kuondoka baada ya kupata fadhila (wema) zake hawana bei.

ਅਮੁਲ ਭਾਏ ਅਮੁਲਾ ਸਮਾਹਿ ॥

Wale waliojikita katika upendo wake hawana bei. Wale waliozama ndani yake hawana bei.

ਅਮੁਲੁ ਧਰਮੁ ਅਮੁਲੁ ਦੀਬਾਣੁ ॥

Amri yake kuu ya Dharma haina bei. Korti yake kuu ya haki haina bei.

ਅਮੁਲੁ ਤੁਲੁ ਅਮੁਲੁ ਪਰਵਾਣੁ ॥

Mfumo wake wa haki hauna bei. Haki iliyo kuu haina bei.

ਅਮੁਲੁ ਬਖਸੀਸ ਅਮੁਲੁ ਨੀਸਾਣੁ ॥

Baraka na zawadi zake hazina bei.

ਅਮੁਲੁ ਕਰਮੁ ਅਮੁਲੁ ਫੁਰਮਾਣੁ ॥

Rehema yake haina bei. Amri yake ya kifalme haina bei.

ਅਮੁਲੇ ਅਮੁਲੁ ਆਖਿਆ ਨ ਜਾਇ ॥

Hana bei, haielezeki.

ਆਖਿ ਆਖਿ ਰਹੇ ਲਿਵ ਲਾਇ ॥

Watu wengi kwa kukariri Naam (neno lake) kwa kutafakari kiundani, wanazama ndani yake Mungu lakini hawawezi kueleza alivyo.

ਆਖਿ ਵੇਦ ਪਾਠ ਪੁਰਾਣੁ ॥

Maandiko matakatifu (Vedas na Puranas) yanamuelezea Mungu.

ਆਖਹਿ ਪੜੇ ਕਰਹਿ ਵਖਿਆਣੁ ॥

Wasomi wanaongea na kutoa mazungumzo kumhusu.

ਆਖਹਿ ਬਰਮੇ ਆਖਹਿ ਇੰਦ੍ਰ ॥

Brahmas na Indras wasiohesabika wanaongea kuhusu Mungu.

ਆਖਹਿ ਗੋਪੀ ਤੈ ਗੋਵਿੰਦ ॥

Krishna (mungu wa wahindi) na wafuasi wake wanaimba sifa zake.

આખહિ ઈમર આખહિ મિય

Shiva (mungu wa wahindi) na Siddhas (watu wenye nguvu za juu) wanamsifu.

આખહિ કેતે કીતે બુધ થી હાજરી હોએ હોએ ॥

Wasomi wengi walioumbwa na yeye wanamsifu.

આખહિ દાનવ આખહિ દેવ ॥

Mashetani na miungu inamtamani.

આખહિ સુરિ નર મુનિ જન સેવ ॥

Watu wengi waliomkubali, mitume watakatifu na wafuasi wao wanaimba sifa zake.

કેતે આખહિ આખણિ પાહિ ॥

Wengi wanamsifu huku wakijaribu kueleza jinsi alivyo.

કેતે કહિ કહિ ઉઠિ ઉઠિ જાહિ ॥

Watu wengi wamemzungumzia mara mara, na wameondoka.

એતે કીતે હોરિ કરેહિ ॥ તા આખિ ન સકહિ કેસી કેએટિ ॥

Kama angeumba vitu vingi zaidi jinsi ambavyo amefanya na kila mtu kushuhudia, fadhila (wema) zake haziwezi kuelezwaa.

જેવ્હં ભાવૈ તેવ્હં હોએટિ ॥

Ni mkuu jinsi atakavyo.

નાનક જાણૈ સાચા સોએટિ ॥

O' Nanak, ni Mungu pekee anayejua alivyo mkuu.

જે કે આખૈ બેલુદિગારુ ॥ તા લિખીએ સિરિ ગાવારા ગાવારુ ॥૨૬॥

Ikiwa mtu anadai kuwa na uwezo wa kueleza jinsi Mungu alivyo, muone kama mtu mpumbavu zaidi.

સે દરુ કેહા સે ઘરુ કેહા જિતુ બહિ સરબ સમાલે ॥

Mungu, ni aina gani ya makao yanaweza kuwepo, ambako unatunzia uumbaji wako, kwa kuwa ukokila mahali?

ਵਾਜੇ ਨਾਦ ਅਨੇਕ ਅਸੰਖਾ ਕੇਤੇ ਵਾਵਣਹਾਰੇ ॥

Katika uumbaji wako, aina nyingi ya miziki ya mbinguni inaimbiwa wewe, huku ikitoa nyimbo zisizo hesabika.

ਕੇਤੇ ਰਾਗ ਪਰੀ ਸਿਉ ਕਹੀਅਨਿ ਕੇਤੇ ਗਾਵਣਹਾਰੇ ॥

Waimbaji wengi wanaimba juu yako katika hatua kadhaa za muziki.

ਗਾਵਹਿ ਤੁਹਨੇ ਪਉਣੁ ਪਾਣੀ ਬੈਸੰਤਰੁ ਗਾਵੈ ਰਾਜਾ ਧਰਮੁ ਦੁਆਰੇ ॥

Upopo, bahari, mvua na moto vyote vinaimba sifa zako kwa sauti zao. Hakimu mwenye haki pia anaimba sifa zako.

ਗਾਵਹਿ ਚਿਤੁ ਗੁਪਤੁ ਲਿਖਿ ਜਾਣਹਿ ਲਿਖਿ ਲਿਖਿ ਧਰਮੁ ਵੀਚਾਰੇ ॥

Malaika wa kihadith au wa kudhaniwa tu, Chitr na Gupt, ambao huweka rekodi ya matendo, na hakimu mwenye haki wa Dharma ambaye husoma matendo hayo, wanaimba kukuhusu.

ਗਾਵਹਿ ਈਸਰੁ ਬਰਮਾ ਦੇਵੀ ਸੋਹਨਿ ਸਦਾ ਸਵਾਰੇ ॥

Shiva, Brahma na miungu ya urembo inayoangaza daima katika utukufu wako wanaimba sifa zako.

ਗਾਵਹਿ ਇੰਦ ਇਦਾਸਣਿ ਬੈਠੇ ਦੇਵਤਿਆ ਦਰਿ ਨਾਲੇ ॥

Hindra ikiwaameketi katika kitit chake cha enzi chenye kuvutia, pamoja na miungu wengine wanakutamani kwa kuomba.

ਗਾਵਹਿ ਸਿਧ ਸਮਾਪੀ ਅੰਦਰਿ ਗਾਵਨਿ ਸਾਧ ਵਿਚਾਰੇ ॥

Sidhas (watu watakatifu walo na nguvu za kiroho) wanakusifu kwa kutafakari kindani kwa heshima. Pia, mitume wanaimba sifa zako kwa kutafakari kwa kina.

ਗਾਵਨਿ ਜਤੀ ਸਤੀ ਸੰਤੋਖੀ ਗਾਵਹਿ ਵੀਰ ਕਰਾਰੇ ॥

Wenye nidhamu, wenye kusaidia wengine, walioridhika na wasioogopa wanaimba sifa zako kwa kuomba

ਗਾਵਨਿ ਪੰਡਿਤ ਪੜਨਿ ਰਖੀਸਰ ਜੁਗੁ ਜੁਗੁ ਵੇਦਾ ਨਾਲੇ ॥

Pandits na wale walio na maarifa ya kiroho ambao kwa muda mrefu wamekua wakisoma Vedas, wanaimba sifa zako.

ਗਾਵਹਿ ਮੇਰਣੀਆ ਮਨੁ ਮੇਰਨਿ ਸੁਰਗਾ ਮਛ ਪਇਆਲੇ ॥

Wanasaji wa kupendeza mbinguni, duniani na katika dunia za jahanamu wanaimba sifa zako kwa kuomba.

ਗਾਵਨਿ ਰਤਨ ਉਪਾਏ ਤੇਰੇ ਅਠਸਠਿ ਤੀਰਥ ਨਾਲੇ ॥

Vitu nya thamani, pamoja na sehemu zote takatifu za haji ulizoumba wewe, zinaimba zifa zako.

ਗਾਵਹਿ ਜੋਧ ਮਹਾਬਲ ਸੂਰਾ ਗਾਵਹਿ ਖਾਣੀ ਚਾਰੇ ॥

Mashujaa wengi, mitume wenye nguvu kubwa ya kiroho na viumbe kutoka kwa vyanzo vyote vinne nya maisha wanaimba sifa zako.

ਗਾਵਹਿ ਖੰਡ ਮੰਡਲ ਵਰਭੰਡਾ ਕਰਿ ਕਰਿ ਰਖੇ ਧਾਰੇ ॥

Mabara yasiyohesabika, mfumo wa jua na sayari zake, na makundi ya nyota, zilizoumbwa na kushikiliwa na wewehi, zinaimba kukuhusu.

ਸੇਈ ਤੁਧੁਨੇ ਗਾਵਹਿ ਜੋ ਤੁਧੁ ਭਾਵਨਿ ਰਤੇ ਤੇਰੇ ਭਗਤ ਰਸਾਲੇ ॥

Wale tu amba owanaweza kuimba sifa zako, wanaokupendeza na wamejitolea kiukweli na upendowakokujikita ndani yao.

ਹੋਰਿ ਕੇਤੇ ਗਾਵਨਿ ਸੇ ਮੈ ਚਿਤਿ ਨ ਆਵਨਿ ਨਾਨਕੁ ਕਿਆ ਵੀਚਾਰੇ ॥

O' Nanak, wengi mnogi wanaimba kukuhusu na hawaji akilini mwangu. Nitawezaje kueleza kuwahu su wote?

ਸੇਈ ਸੇਈ ਸਦਾ ਸਚੁ ਸਾਹਿਬੁ ਸਾਚਾ ਸਾਚੀ ਨਾਈ ॥

Ni Mungu pekee anayeishi milele. Yeye kama mkuu haonekani lakini ni wa kweli, na ukuu wake ni wa milele.

ਹੈ ਭੀ ਹੋਸੀ ਜਾਇ ਨ ਜਾਸੀ ਰਚਨਾ ਜਿਨਿ ਰਚਾਈ ॥

Aliyeumba ulimwengu huu yupo na atakuwepo milele. Hakuzaliwa, na hatakufa.

ਰੰਗੀ ਰੰਗੀ ਭਾਤੀ ਕਰਿ ਕਰਿ ਜਿਨਸੀ ਮਾਇਆ ਜਿਨਿ ਉਪਾਈ ॥

Ameumba Maya wa rangi nyingi, mbegu nyingi na aina nyingi.

ਕਰਿ ਕਰਿ ਵੇਖੈ ਕੀਤਾ ਆਪਣਾ ਜਿਵ ਤਿਸ ਦੀ ਵੱਡਿਆਈ ॥

Kwa kuwa ameumba, anauchunga uumbaji huo kwa ukuu wake.

ਜੇ ਤਿਸੁ ਭਾਵੈ ਸੋਈ ਕਰਸੀ ਹੁਕਮੁ ਨ ਕਰਣਾ ਜਾਈ ॥

Anafanya kinachompendeza. Hakuna yelete anayemuamuru anachofaa kufanya.

ਸੇ ਪਾਤਿਸਾਹੁ ਸਾਹਾ ਪਾਤਿਸਾਹਿਬੁ ਨਾਨਕ ਰਹਣੂ ਰਜਾਈ ॥੨੭॥

Ni mfalme wa wafalme, aliye mkuu; O' Nanak, ni muhimu kuishi kulingana na amri yake.

ਮੁੰਦਾ ਸੰਤੋਖੁ ਸਰਮੁ ਪਤੁ ਝੋਲੀ ਧਿਆਨ ਕੀ ਕਰਹਿ ਬਿਭੂਤਿ ॥

O' Yogi, fanya kuridhika kuwa vipuli vya masikioyako, bidii iwe bakuli na gunialako la kuomba, na kutafakari juu ya neno la Mungu iwe kama jivu linafunika mwili wako.

ਖਿੰਥਾ ਕਾਲੁ ਕੁਆਰੀ ਕਾਇਆ ਜੁਗਤਿ ਡੰਡਾ ਪਰਤੀਤਿ ॥

Ufahamu wa kifo iwe koti lako la viraka; tabia nzuri ya hali ya juu iwe hali yako ya Maisha na imani katika Mungu iwe fimbo/bakora yakoya kutembea.

ਆਈ ਪੰਥੀ ਸਗਲ ਜਮਾਤੀ ਮਨਿ ਜੀਤੈ ਜਗੁ ਜੀਤੁ ॥

Undugu wa ulimwengu uwe dhehebu lako; kudhibiti majoribu yako ndiyo njia halisi ya kutwaa akili na roho yako.

ਆਦੇਸੁ ਤਿਸੈ ਆਦੇਸੁ ॥

Namuinamia yeeye, kwa unyenyekevu namuinamia.

ਆਦਿ ਅਨੀਲੁ ਅਨਾਦਿ ਅਨਾਹਤਿ ਜੁਗੁ ਜੁਗੁ ਏਕੇ ਵੇਸੁ ॥੨੮॥

Anaishi milele, safi,hana mwanzo wala mwisho na habadiliki katika miaka yote.

ਭੁਗਤਿ ਗਿਆਨੁ ਦਇਆ ਭੰਡਾਰਣਿ ਘਟਿ ਘਟਿ ਵਾਜਹਿ ਨਾਦ ॥

O' Yogi, chakula utakachoandaa kiwe ni hekima ya kiroho kuwa Mungu anapatikana kila mahali; huruma iwe mgawanyaji wa chakula, na uruhusu sauti ya mziki wa kiukuu katika kila moyo iwe ndio ngoma utakayotumia kuunda sauti.

ਆਪਿ ਨਾਥੁ ਨਾਥੀ ਸਭ ਜਾ ਕੀ ਰਿਧਿ ਸਿਧਿ ਅਵਰਾ ਸਾਦ ॥

Muumbaji mwenyewe ndiye mkuu wa kila mtu, na uumbaji wake wote ukochini ya usimamizi wake. Kujishughulisha na kufanya miujiza na kutafuta raha zinginezo ni vitu ambavyo vitakuondoa mbele ya Mungu.

ਸੰਜੋਗੁ ਵਿਜੋਗੁ ਦੁਇ ਕਾਰ ਚਲਾਵਹਿ ਲੇਖੇ ਆਵਹਿ ਭਾਗ ॥

Kujunga au kujiondoa kwake hufanyika kwa amri yake. Tunakuja kupokea yaliyoandikwa katika hatima yetu.

ਆਦੇਸੁ ਤਿਸੈ ਆਦੇਸੁ ॥

Namuinamia yeye, kwa unyenyekevu namuinamia.

ਆਦਿ ਅਨੀਲੁ ਅਨਾਦਿ ਅਨਾਹਤਿ ਜੁਗੁ ਜੁਗੁ ਏਕੇ ਵੇਸੁ ॥੨੯॥

Anaishi milele, safi,hana mwanzo wala mwisho na habadiliki katika miaka yote.

ਏਕਾ ਮਾਈ ਜੁਗਤਿ ਵਿਆਈ ਤਿਨਿ ਚੇਲੇ ਪਰਵਾਣੁ ॥

Kwa njia ya ajabu na siri, muumbaji aliumba Maya. (Anatuona sisi, na wanafunzi wake ndio wenye uwezo wa kumuona).

ਇਕੁ ਸੰਸਾਰੀ ਇਕੁ ਭੰਡਾਰੀ ਇਕੁ ਲਾਏ ਦੀਬਾਣੁ ॥

Mungu ni muumbaji, mpeanaji na mwangaminzi.

ਜਿਵ ਤਿਸੁ ਭਾਵੈ ਤਿਵੈ ਚਲਾਵੈ ਜਿਵ ਹੋਵੈ ਫੁਰਮਾਣੁ ॥

Anasababisha mambo kufanyika kulingana na kupenda kwa amri yake kuu. Hivyo ndivyo amri yake ya mbinguni ilivyo.

ਓਹੁ ਵੇਖੈ ਓਨਾ ਨਦਰਿ ਨ ਆਵੈ ਬਹੁਤਾ ਏਹੁ ਵਿਡਾਣੁ ॥

Anachunga vitu vyote, hakuna anayeweza kumuona. Ajabu iliyoje!

ਆਦੇਸੁ ਤਿਸੈ ਆਦੇਸੁ ॥

Namuinamia yeye, kwa unyenyekevu namuinamia.

ਆਦਿ ਅਨੀਲੁ ਅਨਾਦਿ ਅਨਾਹਤਿ ਜੁਗੁ ਜੁਗੁ ਏਕੇ ਵੇਸੁ ॥੩੦॥

Anaishi milele, safi,hana mwanzo wala mwisho na habadiliki katika miaka yote.

ਆਸਣੁ ਲੋਇ ਲੋਇ ਭੰਡਾਰ ॥ ਜੇ ਕਿਛੁ ਪਾਇਆ ਸੁ ਏਕਾ ਵਾਰ ॥

Katika dunia zote kuna viti vyake na magala yake. Kilichowekwa ndani ya magala hayo kiliwekwa mara moja tu.

ਕਰਿ ਕਰਿ ਵੇਖੈ ਸਿਰਜਣਹਾਰੁ ॥

Baada ya kuumba, muumbaji anauchunga uumbaji huo.

ਨਾਨਕ ਸਚੇ ਕੀ ਸਾਚੀ ਕਾਰ ॥

O' Nanak, mfumo wa Mungu wa kudumisha uumbaji wake ni kamilifu.

ਆਦੇਸੁ ਤਿਸੈ ਆਦੇਸੁ ॥

Namuinamia yeYe, kwa unyenyekevu namuinamia.

ਆਦਿ ਅਨੀਲੁ ਅਨਾਦਿ ਅਨਾਹਤਿ ਜੁਗੁ ਜੁਗੁ ਏਕੋ ਵੇਸੁ ॥੩੧॥

Anaishi milele, safi,hana mwanzo wala mwisho na habadiliki katika miaka yote.

ਇਕ ਦੂ ਜੀਭੌ ਲਖ ਹੋਹਿ ਲਖ ਹੋਵਹਿ ਲਖ ਵੀਸ ॥ ਲਖੁ ਲਖੁ ਗੋੜਾ ਆਖੀਅਹਿ ਏਕੁ ਨਾਮੁ ਜਗਦੀਸ ॥

Ikiwa mtu angekua na ndimi elfu mia moja mara ishirini na kukariri neno la Mungu mara nyingi awezavyo kwa kila ulimi, ishara ya kuzama katika jina la Mungu kwa kutafakari.

ਏਤੁ ਰਾਹਿ ਪਤਿ ਪਵੜੀਆ ਚੜੀਐ ਹੋਇ ਇਕੀਸ ॥

Mtu angeungana na Mungu kwa kuchukua hatua hiyo inayofaa (kwa kuachana na ego na kutafakari neno la Mungu kwa kujitolea kwa upendo).

ਸੁਣਿ ਗਲਾ ਆਕਾਸ ਕੀ ਕੀਟਾ ਆਈ ਰੀਸ ॥ ਨਾਨਕ ਨਦਰੀ ਪਾਈਐ ਕੁੜੀ ਕੁੜੈ ਠੀਸ ॥੩੨॥

Baada ya kusikia kuhusu hali ya juu ya roho zilikombolewa kiroho, wale wanaodhani kuwa wanaweza afikia hilo kwa kurudia rudia tu jina la Mungu bila ya kuachana na ego, ni sawa na minyoo wanaotembea ardhini kutarajia kupaa angani. O' Nanak, muungano na Mungu hupatikana tu kwa neema yake. Majivuno ya waongo ni uongo tu.

ਆਖਣਿ ਜੋਰੁ ਚੁਪੈ ਨਹ ਜੋਰੁ ॥

Hatujazaliwa na uwezo wa kuzungumza na kunyamaza na utulivu wa akili, bali ni zawadi kutokakwa Mungu.

ਜੋਰੁ ਨ ਮੰਗਣਿ ਦੋਣਿ ਨ ਜੋਰੁ ॥

Hata kuuliza au kupeana misaada ni zaidi ya uwezo wetu.

ਜੋਰੁ ਨ ਜੀਵਣਿ ਮਰਣਿ ਨਹ ਜੋਰੁ ॥

Hatuwezi kuamua Maisha na kifo. Hatuna uwezo wa kuchagua mahali na wakati wa kuzaliwa, na miaka ya kuishi. Kadhalika, hatuna uwezo wa kuamua mahali,wakatina jinsi ya kuaga dunia.

ਜੋਰੁ ਨ ਰਾਜਿ ਮਾਲਿ ਮਨਿ ਸੋਰੁ ॥

Kimaumbile, akili zetu hazina uwezo wa kujiepusha na fikira za ulafi, nguvu na ego.

ਜੋਰੁ ਨ ਸੁਰਤੀ ਗਿਆਨਿ ਵੀਚਾਰਿ ॥

Hatuna uwezo wa kuafikia mwamsho wa kiroho, kupata maarifa au kutafakari.

ਜੋਰੁ ਨ ਜੁਗਤੀ ਛੁਟੈ ਸੰਸਾਰੁ ॥

Hatuna uwezo tuliozaliwa nao wa kuepuka majaribu ya dunia.

